# SADEC TANZANIA POLYTECHNIC INSTITUTE

Mitindo A, Off Mwanza- Shinyanga Road, Misungwi Town
P. O. Box 100 Misungwi
**MWANZA - TANZANIA**
Email: rector@stapi.ac.tz
Website: www.stapi.ac.tz
Mobile: +255 (0) 655 004212/766 004212


## TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA UALIMU WA ELIMU YA AWALI (CHEKECHEA)

Taasisi ya **SADEC TANZANIA POLYTECHNIC INSTITUTE** iliyoko Mjini Misungwi, Mwanza inatarajia kuanza kuendesha mafunzo ya elimu ya awali ifikapo Januari, 2025 na hivyo basi inatangaza nafasi mbili (2) za kazi ya Ualimu wa Elimu ya Awali (Chekechea) kwa mkataba maalumu.

**Sifa za mwombaji:**

1) Awe na Umri usiozidi miaka thelathin (30).
2) Awe Mtanzania au Raia wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.
3) Awe muhitimu wa cheti, astashahada au stashahada katika fani ya elimu ya awali (Chekechea) kutoka Chuo kinachotambuliwa na Baraza la Elimu ya Ufundi na Mfunzo ya Amali (NACTVET).
4) Awe na ujuzi wa kutimia Kompyuta hususani progamu za MS Word na Excel.
5) Awe na stadi za kutafuta wanafunzi kwa kushirikiana na uongozi wa Taasisi.

**Kituo cha kazi:**

Kituo cha kazi kitakuwa ni Mitindo A, Misungwi Mjini katika mkoa wa Mwanza.

**Kiwango cha mshahara**

Walimu watakoajiriwa na Taasisi watalipwa Mshahara kadri ya makubaliano na Taasisi. Kiwango hicho kitakuwa kinaongezeka kutokana na ubora katika utendaji kazi kwa mwalimu husika.

**Viambatisho katika uombaji wa nafasi ya kazi**

1) Barua ya maombi iliyochapwa kwa kompyuta.
2) Wasifu (CV) binafsi wa mwombaji.
3) Nakala ya cheti cha kuzaliwa iliyohakikiwa na mwanasheria.
4) Nakala za vyeti vya elimu ya sekondari na chuo vilivyohakikiwa na mwanasheria.

Barua za maombi zikiwa pamoja na viambatisho husika zitumwe kupitia njia ya barua pepe ya Taasisi ambayo ni rector@stapi.ac.tz kabla ya tarehe 15 Disemba, 2024. Aidha, waombaji lazima wataje namba zao za simu kwa ajili ya mawasilano zaidi. Waombaji watakaokidhi vigezo tu ndiyo watakaoitwa kwenye usaili katika tarehe itakayotangazwa na Taasisi.

Imetolewa na:

**Eng. Harold J. Mtyana**

**Mtendaji Mkuu wa Taasisi**